

Ukweli Wa Dhambi (The Reality Of Sin)

Na

John Kombo

Ukweli Wa Dhambi (The Reality Of Sin)

Na

John Kombo

November 21, 2013

Ukweli Wa Dhambi

Uhalisia wa Dhambi

Fafanuzi ya dhambi: 1 Yoh. 3:4 ndilo fungu letu la maandiko linaloleta fafanuzi la kibiblia. Yohana alieleza, “*Kila afanyaye dhambi afanya uasi kwa maana dhambi ni uasi.*”

Dhambi = Kutokufanya ambacho Mungu anataka ufanye

Mungu ametoa sheria chanya kwa mwanadamu. Kwa mfano, Yakobo anaagiza, “...*kuwatembelea yatima na wajane katika dhiki zao...* (Yak. 1:27). Hili ni AGIZO CHANYA; kitu ambacho Mungu ametuambia kukifanya. Kama mtu akikataa kufanya hiki, anafanya dhambi dhidi ya sheria ya Mungu.

Dhambi = Kufanya kile anachokikataa Mungu

Mfano wa sheria hasi ingekuwa, “*mwibaji na aache kuiba tena...*” (Efe. 4:28). Hii ni kauli chanya ya sheria, kitu ambacho Mungu ametuambia tusikifanye.

Dhambi ni uchaguzi wa uhuru wa mwanadamu ama kufanya alichokisema Mungu kufanya au kufanya kile ambacho Mungu amekataa.

Dhambi = kuacha Na Kazi

Hii ni njia ya maisha

Neno dhambi linatumika katika Biblia kuelezea njia ya maisha. Kwa mfano, mtu anapoendelea katika matendo ya dhambi kiujumla hufanya kile ambacho Paulo anawaeleza Waefeso kuhusiana na mienendo ya maisha yao ya zamani, “...*ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, ...katika tamaa za miili yetu...na ya nia.*” (Efe. 2:2-3). Yohana anasema huyu ndiye yule “*anayetembea gizani* (1 Yoh. 1:5-10). Waefeso waliishi katika tabia za dhambi ambazo zilikuwa zikifanywa katika mila zao. Hii ilikuwa kabla hawaja ongolewa.

Dhambi ni tendo la kipekee ya maisha

Kuna tafsiri nyingine ya dhambi kama **tendo la kipekee** ambayo Wakristo wanafanya na ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Yohana anasema, “...*kama mtu yeyote akifanya dhambi tunawakili...*” (1 Yoh.

2:1). Hii ni dhambi ambayo Wakristo wanafanya “mara kwa mara” lakini hawaifanyi kama njia ya maisha. Hivyo basi, kuna tofauti kati ya **kuishi katika dhaambi** na **kufanya dhambi**. Mtu asietubu atapoteza roho yake kwa kutenda dhambi. Anayetubu atasamehewa dhambi zake kama akipenda kutubia dhambi zake (1 Yoh. 1:7-9) kuna tofauti kaati ya asiyeamini anayeishi katika dhambi na muumini anayeishi katika dhambi. Asiyeamini atapotea kwa sababu hakutii injili (2 Thes. 1:7-9). Muumini anayeendelea kufanya dhambi atapotea kwa sababu hajatubia dhambi ya kipekee katika maisha (Ebr. 10:26; 1 Yoh. 5:16).

Matokeo Ya Dhambi Ni Utengano Na Kufa

Watu wote wametenda dhambi (Rum. 3:9-10, 23). Dhambi katika maisha ya kila mmoja humtenga mtu na Mungu (Isa. 59:1-2), na katika utengano na Mungu kufa kifo cha kiroho (Rum. 5:12; 6:23). Matokeo ya dhambi ni kutengwa na Mungu ambayo ni kifo cha kiroho; kila tunapofikiria dhambi, hivyo, tunapaswa pia kufikiria kuhusu kifo.

Tunapofanyika Wakristo, hatupotezi uwezo wa kufanya dhambi. Bado tuna uhuru wa kuchagua. Mungu hatufanyi kuwa maroboti. Kwa sababu hiyo Paulo anawahimiza Wakristo, “*tumieni akili wala msitende dhambi.*” (1 Kor. 15:34; Efe. 4:26). Akasema, “*niliuadabisha mwili wangu na kuutiisha...*” (1 Kor. 9:27). Hili ni onyo kwa kila Mkristo kuhusu udanganyifu wa dhambi katika maisha ya mtu.

Wokovu wa Mkristo kama matokeo ya utii wa injili katika ubatizo ni lazima. Wakristo wanapaswa kubaki waaminifu.

Wokovu wa Mkristo utegemeana na yafuatayo kwa kuwa na imani:

- Lazima ashikilie neno la Mungu (1 Kor. 15:2).
- Tunapaswa kuwa waaminifu hadi kufa (Ebr. 3:6).
- Lazima tuendelee katika imani (Kol. 1:23)
- Lazima tuwe waaminifu hata kufa (Ufu. 2:10).
- Lazima tuzae matunda (Yohana 15:1-7)
- Lazima tukae ndani ya Yesu (Yohana 15:4).
- Lazima tutembeee nuruni (Yohana 1:7).

Soma yafuatayo:

- Fil. 2:12.
- 1 Tim.4:16

- Ebr. 3:13

Ndg. John Kombo

Kanisa la Kristo Barut

Nakuru, Kenya

